

KUELEWA MMMMAKUBALIANO HURU/IDHIRI YA BURE, YENYI KUELEWEKA NA MAHITAJI YA KWANZA



Huru/bure inamaanisha jamii wamekubali mradi bila kukazwa wala kusukumwa, bila kutishwa wala kushawishiwa.



Mahitaji ya kwanza inamaanisha kuwa waongozi wa umma (ama inchi/I leta), NGO/ONG ama kampuni wanaoleta mradi, lazima wawe wamepata ruhusa ya jamii (idhini) kabla ya kuanzisha kazi yoyote inayolingana na mradi unaohusika ; inamaanisha pia ya kwamba, jamii inahitaji kupewa mda wa kutosha ili kujifunza na kuelewa mradi kabla ya kufikia kwenyi makubaliano ;



Ruhusa inamaanisha pia ya kwamba msimamo wa jamii unapashwa kuheshimika na wadau/ wengine wote wanaohusika na mradi.

Ujuzi inamaanisha ya kwamba habari zote kuhusu kazi itakayo endeshwa zinajulishwa kwa jamii kwa uwazi kabla hazijaanza, na hizo habari zinahitajika kutolewa katika usawa, ukweli ; tena ziwe habari zenye kupashwa kwa njia iliyo wazi ili jamii waweze kuzielewa.



Makubaliano/idhiri ina maanisha ya kwamba miradi (projeti) inaweza fanyika tu wakati jamii (ama wakaaji) wamekubaliana na kazi na miradi zenye kuwahusu. Jamii wana haki pia ya kukataa makubaliano haya ama kutoa makubaliano ya masharti (yenye kusindikizwa na sharti) ya kugaramia hitaji zao, vipaumbele (ama priorités) zao na wasiwasi wao.

● Habari fulani za muhimu zinazohitajika ni kama :

- asili, ukubwa, mda na wigo (ama upana) wa kila mradi unaoendelezwa ;
- shabaa na lengo za mradi ;
- kutambua mahali pote/ maeneo yanayousikwa kuufanya mradi;
- matarajiyo ya matukiyo razmi ya kiuchumi, kijamii, na kitamadhuni, na mazingira, pamoja na hatari iwezayo kujitokeza ; hivyo hivyo. faida yoyote ya kushirikisha wote ;
- watu wanaofaa kushirikishwa kwa kutekeleza wala kuendesha mradi;
- haki za jamii; na
- taratibu/mipangilio ambayo mradi unaweza kumaanisha.

● Jamii wana haki na uamzi wa kujitafutia ushauri wa kujitegemea kutoka kwa mawikili/wenyisheria, kwa wataalamu wengine ama tena kwa NGO/ONG.

● Mashauriano (ama consultation) na jamii na ushiriki wao ni vitu muhimu saana katika mchakato (kipindi) cha kupata makubaliano. Mashauriano yanapashwa kuwa yenye nia nzuri, hii inashurtisha katika mambo mengine, ya kwamba msimamo (ama mawazo) wa jamii uzingatiwe katika mchakato ama kipindi cha kuendesha kwa mradi, na isipowezekana, inabidi kuwatolea jamii mafasirio kuhusu sababu za lazima zisizoruhusu mawazo ama msimamo wao kuzingatiwa.

Lazima wadau (ama sehemu zote kwenyi mradi) kuleta mchango wao ili kuanzisha mazungumzo itakayowaruhusu wote kutambua suruhisho zinazofaa katika hali ya kuheshimiana na ya ushiriki kamili kwenye nafasi sawa ; na kuelewana pamoja kuhusu tarehe za mwisho kwa kukamata maaamzi. Lazima jamii kwa ujumla (wanaume, wanawake, vijana na wazee) washirikie mazungumzo na uamuzi, zaidi kupitia watetezi wanasheria ama wawakilishi (representants) waliochaguliwa kwa uhuru ama kuwatetea kupita njia za kimila (coutumes) ama taasisi (ngazi) zingine.

✓ SHAHURI KUBWA

Mchakato wa CLIP lazimaihakikishe PACL wanaelewa kwa kweli matokeo ya mradi kwa mambo yenye kuhusika na haki za ardhi na udongo pia na utumidhi ya ardhi (ama jinsi ya kutumikisha udongo) wakati tayari pameanzishwa kulindwa kwa eneo ya ardhi katika sehemu moja kubwa ya pori ya jamii katika wilaya (nafasi) yao. Ikiwa Jamii hawafikii kufahamu mambo haya yote, basi, mchakato utasemwa « Siyo wa kueleweka».



Ikumbukwe pia ya kwamba mchakato (njia) wa CLIP uliofanyikiwa siyo tu yenye imesababisha kufikia makubaliano sahihi (sawasawa) ya mikataba iliyopangwa wala iliyotelezwa; mafanikio ya CLIP lazima zaidi iweze kusababisha uhusiano wa kuaminiana, ili kuitolea IUT msingi mzuri ama wa nguvu, ambao ni wa muhimu kwa mafanikio ya mradi kwa mda mrefu.